
# TUSHIRIKISHANE

Society of the Precious Blood - Province of Tanzania
Issue: November, 2021



## YALIYOMO

1. Yaliyonigusa katika Mafungo ya mwaka
2. Utume mpya katika Jimbo la Rulenge – Ngara
3. Utume mpya katika Jimbo la Mbulu
4. Dada Ombretta – Miaka arobaini Katika Ofisi ya Missioni
5. Taarifa mbalimbali

## DIBAJI

Toleo hili linatupa kwa kina taarifa ambazo nyingi tumezisikia tayari, na lengo lake ni kutufafanulia yaliyojiri katika Provinsi yetu kwa ufasaha zaidi. Mafungo yetu ya mwaka huu yalikuwa ni Baraka ya pekee, kwa tafakari, fursa ya kusali na kupumzika. Wenzetu ambao wameteuliwa kwenda kuanza utume katika majimbo ambayo tumealikwa kwa mara ya kwanza, wanatuelezea jinsi walivyopokelewa na majukumu ambayo yako mbele yao. Tuwaombee ili waanze vema utume huo. Lakini ikiwezekana tuwatembelee ili kwenda kuwatia moyo na kujua kiundani fursa na changamoto wanazokabiliana nazo. Makala inayoelezea utume wa Dada Ombretta Matticari inatuhusu mno kwa maana kazi alizozifanya katika ofisi hiyo ya Missioni ndizo zilizosaidia Wamisionari wetu kufaulu katika kusimika mizizi ya Shirika hapa Tanzania na India.







# YALIYONIGUSA KWENYE MAFUNGO YA MWAKA HUU



*Mafungo kundi la kwanza*

Tunamshukuru Mungu kwa neema na Baraka tulizozipata kwenye mafungo ya Mwaka huu yaliyofanyika St. Gaspar's College kwa makundi mawili: kundi la kwanza kuanzia Jumatatu tarehe 4 Octoba hadi Ijumaa tarehe 8 Octoba; na kundi la pili kuanzi tarehe 11 Octoba hadi Ijuma tarehe 16 Octoba 2021. Tulibarikiwa na neno la Mungu liliopitia katika tafakari za kina na mifano hai kutoka kwa Mhubiri wa Mafungo Mhesh. Pd. Castus Rwegoshora kutoka Jimbo Katoliki la Kigoma. Mhsh. Askofu Mlola ndiye aliyekuwa ameombwa kuhubiri mafungo haya, ila kwa sababu zilizo juu ya uwezo wake ilibidi amtume huyu Padre Castus.



Mwanzoni kabisa Mwezeshaji aliainisha mada ya mafungo ya mafungo kuwa ni: **Mpango wa Uenjilishaji tukisindikizwa na Mt. Yosefu na Mama yetu Bk. Maria** ambao aliwataja kuwa ndio Wanafunzi wa kwanza wa Bwana wetu Yesu Kristo. Alianza kwa kubainisha umuhimu wa Padre na mtawa kujipyaisha ili twende tukazae matunda katika utume. Alitukumbusha kuwa katika mafungo ya mwaka ni nafasi ya kufanya mambo makuu matatu: Kutafakari neno la Mungu, Kusali na Kupumzika. Kweli ratiba aliyopendekeza ilikuwa inatupa nafasi ya Kutafakari Neno la Mungu kwa pamoja na kwa binasfi, pia kusali pamoja na sala za binafsi.

Mafungo yaliongozwa na kauli mbiu toka kwenye Injili ya Luka: *"Roho wa Bwana yu juu yangu, kwani ameniweka*

*wakfu, niwaletee maskini habari njema. Amenituma niwatangazie mateka uhuru wao, na vipofu watapata kuona tena, amenituma niwakomboe wanaoonewa, na kutangaza mwaka wa neema ya Bwana." (Lk. 4:18-19).* Alisema kuwa kama huu ndio mpango wa Utume wa Bwana nasi hatunabudi kuamsha upya ndani yetu moyo huu wa utume. Katika siku ya kwanza, aliweka msisitizo juu ya utambulisho wetu (identity), ya kwamba sisi ni Wamisionari tuliotumwa kwenda kutangaza mwaka wa Bwana uliokubalika, tunapaswa kujitambua sisi ni akina nani na kila leo kuishi utambulisho wetu. Alikemea tabia ya baadhi ya Mapadre na watawa kuishi kama watu wa mtaani, akasema: japokuwa msemo wa "Habitus non facit monacus", Vazi la kitawa halifanyi mtu kuwa mtawa ila tabia na maisha ya ushuhuda. Alisisitiza juu ya utambulisho wetu kama wafuasi wa Kristo wanaotambulikana kwa fadhila ya Upendo.

Jambo la pili lilonigusa, katika mengi aliyofundisha, ni kutukumbusha kuwa kuna wahusika watano wakati wa Mafungo. Mhusika wa kwanza ni Roho Mtakatifu, alisisitiza na kutukumbusha kumwomba **Roho Mtakatifu** atuongoze tupate kutafakari, kusali na kujipyaisha. Mhusika wa pili ni **mfungaji** mwenyewe: alisisitiza juu ya umuhimu wa kusikiliza yale ambayo Mungu anataka kutuambia ili mwisho wa mafungo tutoke tukiwa tofauti na tulivyoanza. Mhusika wa tatu ni **Kiongozi wa Mafungo** ambaye ana wajibu wa kushauri na kuchokoza tafakari zinazoweza kutuletea mabadiliko chanya. Mhusika wanne ni **Adui shetani** anayepanda magugu ndani ya shamba (Mt. 13:24-30).

Mtu anaweza kuwepo kwenye mafungo kimwili lakini roho na akili zake ziko mbali. Alitukumbusha kuwa macho na shetani anayeweza kututeka tusifaidi matunda ya mafungo. Mhusika wa tano na wa mwisho ni **Kanisa la tunakotoka** ambalo wakati wote wa mafungo wanatuombea ili Mafungo yetu yawe wakati wa neema. Mwishoni alisisitiza kuwa matunda ya mafungo yanategemea jinsi ulivyo panda na kupalilia. Jiulize, mwaka huu umevuna nini katika mafungo ya Mwaka??

## KAZI YA KUTANGAZA MWAKA WA BWANA INAONGOZWA NA ROHO AMTAKATIFU:

Siku ya Tatu na ya nne ilipambwa na tafakari juu ya Mhusika wa kwanza wa mafungo, yaani Roho Mtakatifu. Kwanza kabisa toka siku ya kwanza tulianza kwa kuimba beti za Sekwensia ya Roho Mtakatifu kabla ya kila tafakari. Katika siku ya tatu Mhubiri alisisitiza juu ya Nguvu zitokazo kwa Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu: *"Bila nguvu zako wewe mwanaamu hana kitu kwake yote yanakosa."* Kwa nukuu nyingi kutoka Biblia takatifu Mhubiri alifafanua umuhimu na kazi za Roho Mtakatifu. Alianza kwa kuhusisha mada ya mafungo na Roho Mtakatifu akionyesha kuwa toka mwanzo wa maisha na utume wa Yesu Roho Mtakatifu aliongoza kila hatua. Yesu alizindua mpango wake wa ukombozi kwa kubatizwa na Roho Mtakatifu, ni Roho huyohuyo aliyemsukuma jangwani ili ajaribiwe. Yesu alipimwa na akashinda na akaanza utume wake akiongozwa na Roho Mtakatifu (Lk. 4:14-19). Mimi na wewe tumepakwa mafuta na Roho Mtakatifu, ndiye anayesukuma utume wetu na kuongoza kila kitu, kwani anajua maana na kuvipa vyote maana. Tunahitaji kuibua upya Roho Mtakatifu ndani yetu na ndani ya Kanisa. Tunahitaji Pentekoste mpya ambayo sio tofauti na ile ya kwanza (Mdo 2,4-8; 4,31; 2Kor. 4,16). Alisisitiza juu ya umuhimu wa kumkaribisha Roho Mtakatifu katika maisha yetu ya kila siku na kwenye mipango yetu.

## MAISHA YA UTUME NA UHUSIANO NA BK. MARIA:

Mhubiri wetu alitoa ushuhuda kuwa katika maisha na utume wake Ibada kwa Mama Bk. Maria imekuwa nguvu kubwa ya kiroho na akashauri nasi tuwe na ibaada kwake na hatutakosa msaada wa maombezi yake, Mama wa Kristo ambaye amekabidhiwa kwetu na Bwana wetu Yesu Kristo pale msalabani. Alisisitiza kuwa Maria ni kielelezo cha ufuasi wa Yesu kwa namna nne. Kwanza kabisa **Maria Mama yetu ni kielelezo cha utii wa kienjili.** Akafafanua kwamba Utii kwa Mapadre wa jimbo wanautoa kwa Askofu wakati Watawa wana kiapo cha utii kupitia mkuu wa shirika. Aina zote mbili zinapata mfano toka kwa Maria Mama wa Yesu kupitia ile NDIYO ya kwanza alipokubali Kazi ya kumleta Ulimwenguni Mkombozi (Lk. 1, 38). Maria aliutimiza wito wake kiaminifu hadi mwisho na diyo maana anasema: *"tokea sasa watu wote wataniita Mwenye heri"* (Lk.1,48). Lakini pia Maria ni kielelezo cha Usafi kamili kwa maana yeye amekuwa mkarimu katika kutimiza Matakwa ya Mungu kiaminifu. Akifafanua hili alisisitiza kuwa usafi wa moyo ni mtindo wa maisha na ni zaidi ya kujinyima, zaidi ni kujitoa kuwapenda wenzetu. Zaidi sana **Maria ni kielelezo cha sala.** Kwa kuwa Maria alikuwa anasali ndiyo maana aliweza kutambua na kupokea mapenzi ya Mungu kwa furaha, alisisitiza Mhubiri wetu. Alifafanua kwamba mtu mwenye kupurukusha sala anajikuta mkavu kwa sababu sala ni msukumo wa utakatifu. Alituhimiza kila siku kukutana na Mungu kabla ya kukutana na watu katika utume. Kwa mifano mbalimbali alitushauri tuwe watu wa sala ya kuabudu Ekaristi, sala ya ukimya na zaidi tuwe na udumivu katika sala. Mwisho alibaini kuwa Maria mama yetu ni kielelezo cha shukrani. Ni kweli tunapoadhimisha sadaka ya Misa tunamtolea Mungu shukrani zetu na katika hilo Maria ni Mater alter Christus, alisisitiza mhubiri wetu.

## HITIMISHO:

Katika kuhitimisha aliorodhesha mambo sita ambayo ndiyo yatakayotusaidia kutunza neema tuliyopata katika mafungo yetu nayo ni:

1. Daima tuhesabiwe watumishi, kamwe tusitumikie kwa kujitutumua
2. Tuweke katika ratiba zetu kuabudu Ekaristi Takatifu kwani pale ndipo tutaomba na kupewa fadhila mbalimbali lakini hasa ile ya unyenyekevu na usafi kamili. Katika Tabernacle ndiko chemchemi ya cheche za utume (1Kor. 14, 20).
3. Tujitahidi tuwe na Mwongozi wa kiroho, Padre au mtu ambaye kwake tutaweza kujifunua na anayeweza kutuambia ukweli bila kuogopa.
4. Tuungame kila mara, ndiyo njia ya utakatifu
5. Tusiwe watu wagumu, tuwe flexible katika maisha na utume wetu.
6. Tuwe watu wa kujisomea na kujifunza kabla ya kuhubiri: Tujifunze mambo mapya, tusiridhike na yale tunayoyajua tayari. Tuhubiri maada ya maandalizi ya kutosha na sio kukurupuka







*Mafungo kundi la pili*

# UTUME MPYA KATIKA JIMBO LA RULENGE-NGARA: PAROKIA YA MT. JOSEPHINA BAKHITA-BENACO

Na Pd. Deusdedit Mulokozi, C.PP.S.

Tarehe 25 Septemba ya mwaka 2021, itabaki katika kumbukumbu za kihistoria kwenye Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi ya Bwana wetu Yesu Kristo, Provinsia ya Tanzania; kwamba ndiyo siku ambapo ilifunguliwa jumuiya mpya katika jimbo la Rulenge-Ngara. Mbele ya viongozi waandamizi wa Askofu, Halmashauri ya walei Parokia, masista wa Fransiskani wa Mtakatifu Bernadeta wa Lurdi, mapadre wa jimbo, baadhi ya mapadre wa shirika, na baadhi ya waamini, Baba Askofu wa jimbo, Severine Niwemugizi, alimkabidhi mkuu wa Shirika Fr. Vedasto Ngowi, C.PP.S, parokia ya Mt. Josephina Bakhita-Benaco. Baada ya makabidhiano hayo ilifuata ibada fupi ya kumsimika rasmi paroko mpya wa Parokia hiyo. Kwa hiyo jumuiya hiyo inaundwa na Padre Deusdedit Mulokozi C.PP.S (Paroko), na Padre Innocent Miku, C.PP.S, (Wakili Paroko).

Ibada fupi ilipomalizika wote waliokuwepo walikaribishwa kwenye chakula pamoja na Baba Askofu. Zoezi hili halikuchukua muda mrefu sana kwani baadae ilitakiwa kupitia ripoti ya makabidhiano ili kuona kama kila kitu kilichotajwa kwenye ripoti hiyo kipo katika uhalisia wake.

Parokia ya Mt. Josephina Bakhita-Benaco ilitangazwa parokia teule mnamo Mei, 2011 na kuzinduliwa rasmi kuwa parokia tarehe 10/03/2017. Parokia hii ina vigango 15, kati ya hivyo ni vigango 8 tu vinavyofikika kwa gari muda wote, vilivyobaki ni kwa njia ya pikipiki tu, na wakati wa mvua utume husimama hadi kiangazi. Hali za vigango zinatofautiana kulingana na mazingira na watu wanaounda vigango hivyo. Benaco

ni eneo linaloundwa na watu toka sehemu mbalimbali. Hii inatokana na historia ya kuundwa kwake. Kabla ya mauaji ya kimbari ya Rwanda ya mwaka 1994, eneo hili lilikuwa kwa sehemu kubwa ni pori. Lakini baada ya wakimbizi kupata hifadhi maeneo haya watu toka sehemu mbalimbali walihamia hapa kwa lengo la kujipatia fursa. Baada ya wakimbizi kurudi makwao wengi wa makundi haya walibaki na kuendelea na shughuli za biashara, kilimo na ufugaji.


Miundo mbinu ya vigango ni hafifu kwani yapo makanisa ya nyasi juu na chini, matope na juu majani, miti na juu mabati, matofari na juu mabati na vile ambavyo havina majengo bali waamini husali chini ya miti au wanatumia majengo ya shule. Kigango cha mwisho kipo umbali wa kilometa 60. Kigango hiki hupata huduma kipindi cha kiangazi kwa pikipiki tu. Parokia ina jumla ya waamini 5,679 kadili ya sensa ya 2017, na kati ya hao ni 1,500 walio hai. Mbali na changamoto hizo bado waamini wanaonekana kuhitaji wachungaji. Kwa sala na sadaka zetu tuendelee kushikamana ili utume huu kwa familia ya Mungu uweze kuleta matumaini na ndoto ya Mt. Gaspari iendelee kudhihirishwa kwa njia ya utume wetu. Mungu awabariki!





# UTUME MPYA KATIKA JIMBO LA MBULU: PAROKIA YA MT. YUDA THADEI – GUNYODA

Na Pd. Bonaventure Mushi, C.PP.S.



Tushirikishane... Ndoto ya Mt. Gaspari ya kutaka kufahamu lugha elfu imeendelea na sasa katika Jimbo Katoliki Mbulu kufuatia ombi la Askofu Anthony Lagwen. Wamisionari wa Damu Takatifu ya Yesu wamefika rasmi Jimboni Mbulu kwa utume Ijumaa ya tarehe 08 Octoba 2021 saa nne asubuhi. Tukiongozwa na Mkuu wa shirika Pd. Vedasto Ngowi CPPS na Mhasibu Pd Dominic Mwaluko, CPPS. Tulipokelewa vizuri na Askofu na baada ya mazungumzo mafupi tuliendelea na safari fupi kuelekea kwenye Parokia aliyoomba Shirika kufanya utume.

Tuliwasili katika Parokia ya Mt. Yuda Tadei, Gunyoda

muda wa saa sita hivi na baada ya sala na utambulisho makabidhiano yalianza kati ya Paroko aliyekuwa anahama na Wamisionari wa Damu Azizi. Haya yalifanyika mbele ya uongozi wa jimbo na Shirika pamoja na Halmashauri ya walei Parokia. Parokia ya Mt. Yuda Tadei ipo eneo linaloitwa Gunyoda, katika halmashari ya mji wa Mbulu. Ni kilomita 13 toka mjini Mbulu. Parokia hii ilizaliwa mwaka 2004 toka Parokia ya DAWDI ambapo waliinjilishwa na kuhudumiwa na shirika la Ndugu wadogo Wakapuchini (OFM Cap). Parokia ilipozaliwa ikaanza kuhudumiwa na mapadre wa Jimbo kwa ushirikiano na mapadre Wakapchini OFM Cap. Tulipowasili hapa katika macho ya wakristo na viongozi walei ni kama usiku mrefu umekwisha, jua limechomoza. Wamekuwa na shauku kubwa kuona mabadiliko yanatokea. Ni watu wazuri wenye imani na rasilimali nyingi. Shida kubwa waliopata ni kukosa Mchungaji wa kuwasikiliza, kuwaongoza na kuwahamasisha hasa ukizingatia sehemu kubwa ni wafugaji na wanajua mchungaji ni nani. Parokia ina vigango 11 vilivyounganishwa na kutengeneza kanda tatu (3) ili kurahisisha huduma. Na kanda zote hizi zina makanisa yenye Ekaristi takatifu ndani na nyumba ya Padre. Idadi ya wakristo ni zaidi ya 4,000/- Makabila ya hapa ni Wairaqw, Wamang'ati na kabila ndogo la Wahdzabe. Hitaji kubwa kwa sasa ni Uinjilishaji na uhamasishaji wa shughuli nyingine za maendeleo. Wakristo wana kiu kubwa ya huduma za kiroho ambapo inahitaji mapadre angalau wawili kwa uchache. Ndoto ya Mt. Gaspari del Bufalo, Inaendele

## DADA OMBRETTA - MIAKA 40 KWENYE OFISI YA MISIONI – ITALIA

Na: Ombretta Matticari



*Karibu umfahamu Dada Ombretta ambaye amefanya kazi kwa miaka Arobaini katika ofisi ambayo ilikuwa ikiratibu shughuli za Wamisionari wa Provinsi ya Italia waliokuwa wanafanya utume nchi za nje, hasa amefanya mambo mengi kwa ajili ya utume wa Mission yetu ya Tanzania toka 1982-2021.*

Baada ya kumaliza masomo ya Sekondari kama vijana wengi wa wakati wangu, unakuwa hujui maisha yako ya kazi yatakuwaje; la msingi ni kupata kazi bila kujua ni hali ipi utakayokutana nayo. Nilijua toka mwanzo kuwa nisingeweza kuendelea na masomo ya chuo kikuu, na ndio maana nilinuia kutumia kila fursa itakayojitokeza. Hivyo ndivyo ilivyokuwa,

na mwaka 1982 nikakutana na Wamisionari wa Mt. Gaspari ambao walihitaji mtu wa kufanya kazi ya Ukatibu masijala katika ofisi iliyokuwa ikishughulikia Utume wan chi za nje ya Italia. Ndivyo nilivyoanza kazi katika Ofisi ya Missioni bila kujua maisha yangu ya mbeleni yatakuwaje.

Nilianza kazi kwa ari na nia moja sikujua ni mambo yapi nitakutana nayo katika adventure hii, kwangu yote yalikuwa kama fumbo. Ndivyo nilivyokuwa naangalia kazi yangu ambayo mambo yote yalikuwa mageni na ya kustaajabisha maana viongozi wangu walikuwa Mapadre. Mwanzoni nilianza kupanga makabrasha ya ofisi hii bila kujua maudhui na makusudi yake. Baada ya muda na baada ya kupata maelekezo juu ya malengo ya ofisi hii nilianza taratibu kupanga majukumu na shughuli ambazo ilibidi zipitie katika ofisi hii. Katika hili viongozi wangu wa kazi, Wamisionari waliopitia katika kazi hii waliendelea kunitia moyo na kwa njia hii niliwajibika kwa mahitaji ambayo yalibidi kukidhiwa kwa ajili ya kazi za kitume zilizokuwa zikifanyika katika nchi za nje, hasa Tanzania. Sehemu hii ya mwanzo wa kazi zangu ilihitaji, umakini mkubwa, utafiti wa kina na kuwajibika kwa masaa mengi hata mara nyingi muda wa ziada ulihitajika.

Katika kufanya kazi hii nilikutana na Tanzania, nikajifunza kuifahamu hata kabla ya kufika huko. Kwangu ilikuwa nchi ya kigeni na hasa nchi ya kiafrika yenye matatizo yake, kwangu mbali lakini nilijifunza kuiona kuwa nchi ambayo ilikuwa karibu kabisa na utume wa Wamisionari niliofanyakazi nao. Hao Mapadre ndio walioniingizia moyoni nchi hii ya kigeni ambayo Mt. Gaspari alikuwa amekusudia mengi kwa ajili yake kwa kupitia mapadre na walei wengi waliokuwa wakienda na kurudi kutoka nchi hiyo, wakiwa wajaa hamasa ya kufanya mengi kwa ajili ya upendo.

Hivyo basi ofisi hii taratibu ikawa ni kItuo cha kupanga na kuratibu mahitaji mbalimbali ambayo Wamisionari walikuwa wakiyahitaji kwa utume. Vitu mbalimbali hasa vile ambavyo kule Tanzania ilikuwa ni vigumu kuvipata vilikusanywa na kutafuta namna ya kuvisafirisha. Ofisi ikawa kama kituo cha safari za kimisionari kwa mapadre na walei waliokuwa wakienda kujitolea kuboresha maisha ya watu hao. Japokuwa hakukuwa na njia za kisasa za mawasiliano ofisi niliyokuwemo ikawa ni kituo cha kuunganisha nchi hizi mbili, tukitumia njia zilizokuwepo: simu, Telefax, Telex na radio calls.

Pamoja na mabadiliko ya Wakurugenzi wa ofisi hii na Wahazini wa Provinsi, kadiri miaka ilivyopita mimi niliendelea kufanya kazi yangu kwa dhamira na bidii ileile. Wale wote ambao walikuwa wanahusika na miradi mbalimbali kwa ajili ya utume wa nchi za nje ya Italia, walikuwa wakifanya kazi karibu nami na tukafanya kazi hii kama yetu. Ujenzi wa Hospitali ya Mt. Gaspari Itigi, na kazi mbalimbali za kuiwezesha iendelee kutoa huduma zake kwa ufanisi, haikuwa kazi rahisi. Kwa misaada ya hali na mali toka kwa watu wakarimu iliuwezesha mradi huu kuwa ni kati ya miradi mikubwa na ya muhimu kwa Shirika la Mt. Gaspari.

Naweza kusema kuwa nikiwa katika ofisi hii nilipata fursa ya kukutana na watu wengi wema na wakarimu, wenye moyo wa upendo: Mapadre, Masista, walei, Madaktari manesi mafundi wa aina mbalimbali wajenzi na watu wa fani mbalimbali. Kuliundwa ushirika wa watu wenye moyo wa namna hiyo lakini pia makundi na mashirika yasiyo rasmi na NGO ambayo kwa moyo waliunga mkono juhudi za Wamisionari walizokuwa wakifanya Tanzania na kwingineko. Walikuwa wakienda huko na wakirudi unawaona wamebadilika, kama vile mang'amuzi yao yalikutana na ulimwengu

mpya uliogusa mioyo yao unaowaalika kufanya zaidi.
Leo hii huko Tanzania kuna majengo, miradi na taasisi nyingi ambazo ni matunda ya miaka arobaini ya juhudi za watu hawa wote ambao ni wafadhili toka Italia, Kanada na nchi nyinginezo. Lakini pia ni matunda ya juhudi za Wamisionari Watanzania ambao wameisimamia na kuhakikisha inakuwa faida kwa watu wao. Kwa upande wangu naona fahari kuwa sehemu ya haya yote yaliyotendeka nikiwa katika ofisi hii ya Misioni, nikishirikiana kwa bidii na Mapadre wa Mt. Gaspari kutimiza ndoto za mwanzilishi wao. Mwaka huu mwezi wa July nimestaafu, najisikia simanzi moyoni, ila nimeacha nyuma urithi mkubwa wa kujivunia. Namshukuru Mungu kwani nimeondoka na roho tajiri ya Umisionari na heshima toka kwa wote niliobahatika kushirikiana nao katika utume huu. Nawaombea wote ili katika maisha yenu mpate kazi na utume kama niliobahatika kufanya. Utume huu umekuwa faraja kwangu katika nyakati za shida na nyakati za furaha katika miaka arobaini niliyofanya kazi katika Ofisi hiyo, nikisaidiwa kuvuka vizingiti nilivyokutana navyo.
Ninawashukuru na kuagana na kila mtu kwa Upendo!

# TAARIFA MBALIMBALI

## Pd. Evarist Lefiyo ahitimu masomo yake:



Mnamo Tarehe 19 Octoba 2021, Pd. Evarist Lefiyo amehitimu rasmi masomo yake ya Shahada ya Sheria. Mahafali yalifanyika katika Chuo kikuu cha Dar-es-salaam, na yalikuwa ni mahafali ya 51. Pd. Evarist alisindikizwa na wanajumuiya wenzake katika kusherekea na kumshukuru Mungu kwa kutimiza ndoto yake ya muda mrefu. Pd. Lefiyo ni wa pili katika Shirika



kuhitimu masomo ya sharia (Civil Law) wa kwanza alikuwa Pd. Denis Mlimira ambaye kwa sasa anaendelea na masomo ya uzamili katika fani hiyohiyo. Tunao pia Wana Sheria wa Sheria za Kanisa: Fr. Dr. Richard Tiganya anayefundisha katika

Seminari ya Segere na Pd. Richard Orota. Tunamtakia Pd. Evarist utume uliotukuka katika kulisaidia Shirika katika mambo yanayohitaji taaluma yake.

## Pd. Thomas T. Kilewona aadhimisha Jubilei ya fedha:


Mnamo tarehe 7 Octoba Pd. Thomas Temba aliadhimisha Jubilei ya fedha ya Upadrisho wake. Sherehe hiyo ilifanyika katika Parokia yake ya kuzaliwa – Parokia ya Shimbwe Jimbo Katoliki la Moshi. Pd. Ladislaus Maliwa wa Shirika la Wa Rosmini naye mzaliwa wa parokia hiyo hiyo, aliadhimisha pamoja na Pd. Kilewona. Mungu azidi kujamia miaka mingi ya utume.





## Pd. Felix Mushobozi aadhimisha Miaka thelathini ya Upadre:

Ilikuwa siku ya Jumatano tarehe 29 Septemba 2021, wakati Kanisa linaadhimisha Sikukuu ya Malaika Wakuu, Pd. Felix pamoja na Wamisionari wa Kanda ya Dodoma aliadhimisha Misa ya Shukrani kwa zawadi ya wito wa upadre Mmisionari pale kwenye nyumba ya Malezi Miyuji Dodoma. Baada ya Misa takatifu tafrija fupi ilifanyika na ikapambwa na uwepo wa Watawa kutoka nyumba za jirani.





## Kigango cha Mkiwa kuwa Parokia teule:

Baba Askofu Edward Mapunda ameamua kukifanya Kigango cha Mkiwa kuwa Parokia teule. Kwa barua yake kwa Mkuu wa Provinsi ya Tanzania Pd. Vedasto Ngowi Askofu ana nia ya kukifanya kigango cha Mkiwa kuwa Parokia ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Miaka 50 ya kuanzishwa jimbo la Singida. Utume na Uchungaji wa Parokia teule ya Mkiwa utakabidhiwa kwa Pd. Alessandro Manzi atakihudumia akitokea kwenye jumuiya ya Itigi, na kutoa huduma za kiroho kwa nyumba ya Masista wa Mt. Ursula Mkiwa.




*Kanisa*



*Nyumba ya Mapadre*

## Br. Andrea Velocci – Mwanajumuiya ya Hospitali ya Mt. Gaspari Itigi:



Huyu ni Bruda pekeealiyebaki wa Province ya Italia ambaye amechagua kufanya utume wake kati yetu hapa Tanzania. Br. Adrea aliingia shirikani rasmi na kwa daima tarehe 4 July 2021 na amefika Itigi kuanza utume wake tarehe 15 Agosti 2021. Hivi karibuni, yeye ataanza rasmi masomo ya Uuguzi katika Chuo chetu cha uuguzi Itigi na atakuwa kiunganishi kati ya Uongozi wa Hospitali na Province ya Italia.

## Wamisionari Watatu waenda Austria kwa Utume:

Pd. Stephano Karabyo, Pd. George Mwaluko na Pd. Godfrey Boge wameondoka tarehe 7 Novemba kuelekea Austria katika mji wa Salzburg kwa kujiunga na Wamisionari wenzetu wa Teutonic Province kwa utume. Wamisionari hawa watatu kwa mwaka mzima walikuwa wakijiandaa kwa kazi hii wakijifunza lugha na utamaduni wa huko. Wakifika huko pia wataendelea kujifunza hadi waingie katika jadi na utamaduni wa kijerumani. Tunawaombea utume uliotukuka.



# UTEUZI NA UHAMISHO

**Fr. Dennis Pantaleo Massawe** ateuliwa kusimamia Shrine ya Mt. Gaspari Mbezi. Baada ya matibabu yake yaliyochukua takribani mwaka mzima, hatimaye Pd. Dennis amehamishiwa katika Jumuiya ya Parokia ya Mt. Gaspari Mbezi Beach. Uteuzi huo unaanza mara.



**Pd. John Makarius Ikelesho** anahama kutoka Jumuiya ya Mtongani kwenda kwenye Jumuiya ya Manyoni. Huko atakuwa administrator kwa miradi ya Manyoni.



**Pd. Faustino Maganga** ameteuliwa kuwa Paroko wa Parokia ya Mt. Nicholaus Mtongani badala ya Pd. Seventine Banulirwa ambaye atahamia Itigi. Pd. Faustino atasimamia Shule yetu ya ufundi.



**Pd. Philbert Manyama** amehamishwa kutoka jumuiya ya Manyoni kwenda Jumuiya ya Parokia ya Bk. Maria Mama wa Damu Azizi ya Yesu Kisasa. Hapo atafanya kazi kama Msaidizi wa Paroko.



**Pd. Seventine Banulirwa** amehamishiwa kwenye jumuiya ya Itigi baada ya kuhudumia Parokia ya Mtogani



Kwa maoni, ushauri na mapendekezo juu ya toleo hili, wasiliana na:-

Provincial Secretary

cppstzprovince@gmail.com

www.preciousbloodtz.org

C.PP.S PROVINCE OF TANZANIA